# Kuipata na Kuitunza Kesho Yetu Kupitia Ushirikiano wa Kimataifa

Mpango wa Ushirikiano wa Kimataifa wa UCC 2024-2028

Profesa Ursula Kilkelly

Makamu wa Rais wa Ushirikiano wa Kimataifa



University College Cork, Ireland
Coláiste na hOllscoile Corcaigh

# Utangulizi

Chuo Kikuu cha Cork ni chuo kilichojikita katika utafiti chenye mtazamo wa kimataifa, na lengo la kimkakati la kuimarisha hadhi yake na kuongeza mchango wake kimataifa.

Tukijenga juu ya miongo kadhaa ya kufanya tafiti, programu zetu na jumuiya yetu kuwa ya kimataifa, huu ni mpango wa kwanza wa Chuo wa ushirikiano wa kimataifa, unaowasilishwa na uongozi wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Ushirikiano wa kimataifa Profesa Ursula Kilkelly. Ukija wakati ambapo kuna changamoto kubwa ambazo hazijawahi kushuhudiwa duniani, Mpango huu una nguzo nne za azma ya Chuo:

- Ubora wa Kimataifa
- Mchango Duniani
- Ushirikiano wa Kimataifa
- Uraia Mwema Duniani

Ukiongozwa na tunu za Chuo na ukitokana na maoni ya kina ya wadau, Mpango huu wa Ushirikiano wa Chuo unajikita katika ushirikiano wa kimataifa wenye misingi ya kimaadili ambapo utaalamu, rasilimali na sifa za chuo vitatumika kutoa mchango kutatua changamoto kubwa za dunia. Ukiwa umejikita katika taarifa za utafiti, mifumo mipya ya matumizi ya rasilimali na mfano thabiti wa uongozi na utawala bora na jumuishi, Mpango huu unaweka hatua 5 za kipaumbele chini ya kila moja ya nguzo 4 zilizotajwa hapo juu, ukifuatiwa na programu za kazi za kila mwaka zenye malengo yanayopimika ili kufuatilia utekelezaji mwaka hadi mwaka. Kwa asili yake, Mpango wetu wa Ushirikiano wa Kimataifa unakusudiwa kuwa endelevu na wenye uwezo wa Kwenda na mabadiliko ya dunia inayotuzunguka.

Mpango huu unatumia mbinu ya pamoja na jumuishi ya "Chuo Kimoja" iliyobuniwa ili kutumia kikamilifu rasilimali za Chuo chetu kwa ufanisi ili kufanikisha utofauti na ubora.

Natarajia kushirikiana na wanafunzi, walimu, wafanyakazi na wadau wote wa ndani na nje kutimiza azma ya mpango huu.

**Profesa Ursula Kilkelly**
Makamu wa Rais wa Ushirikiano wa Kimataifa
26 Novemba 2024

# Nguzo 4 za Ushirikiano Wetu Kimataifa

## 1. Ubora wa Kimataifa

UCC itanufaika kuwa na wanafunzi na walimu mahiri kutoka nchi mbalimbali duniani ili kuendana na dhamira yake ya ubora na utofauti anuai.

## 2. Mchango duniani

UCC itatoa mchango katika kutatua changamoto kubwa za dunia kupitia utafiti wake, ushirikishi wa wahitimu wake wa zamani, na uongozi wa maarifa katika nyanja mbalimbali.

## 3. Ushirikiano wa Kimataifa

UCC itakuwa mshirika wa kimkakati na wa kimaadili, tukitumia mitandao na washirika wetu kuinufaisha dunia.

## 4. Uraia Mwema Duniani

UCC itaendeleza Uraia Mwema duniani katika elimu, utafiti na ushirikiano, ili kukuza maelewano ya pamoja miongoni mwa watu duniani.

# 1: Ubora wa Kimataifa

UCC itanufaika kuwa na wanafunzi na walimu mahiri kutoka nchi mbalimbali za dunia kuendana na dhamira yake ya kuwa na ubora na utofauti anuai.

## Hatua za kipaumbele

## Tumedhamiria

1. Kuimarisha sifa na mchango wetu kimataifa kupitia uundaji na utekelezaji wa mtindo mpya jumuishi wa mawasiliano na utangazaji wa chuo chetu..

2. Kutumia mfumo ulioratibiwa na unaoongozwa na takwimu katika uandikishaji wa wanafunzi wa kimataifa ili kuimarisha utofauti anuai na ubora wa jumuiya yetu ya Chuo.

3. Kuwapa wanafunzi wa kimataifa uzoefu mzuri katika safari yao yote ya kielimu inayoonesha kujali kwetu mafanikio ya kiwango cha juu cha wanafunzi.

4. Kuimarisha programu zetu pacha na za pamoja na washirika wetu wa kimataifa kwa mujibu wa vipaumbele vyetu vya kimkakati.

5. Kuunga mkono Mpango wa Watu na Utamaduni ili kuvutia vipaji bora vya kimataifa, kuhakikisha Chuo kinajulikana kwa utofauti anuai na ubora wa walimu na wafanyakazi wetu.

# 2: Mchango Duniani

UCC itatoa mchango katika kutatua changamoto kubwa za dunia kupitia utafiti wake, ushirikishi wa wahitimu wake wa zamani, na uongozi wa maarifa katika nyanja mbalimbali

## Hatua za kipaumbele

## Tumedhamiria

1. Kuendeleza mchango wetu katika kutatua changamoto za dunia kwa kuweka kipaumbele katika ushirikiano wa tafiti za kimkakati.

2. Kusukuma mbele nafasi ya chuo katika viwango vya kimataifa, kwa kuweka kipaumbele katika ushirikiano wa kimkakati katika tafiti.

3. Kupanua wigo wetu wa kidunia kupitia mpango mkubwa unaoshirikisha wanafunzi wetu wa zamani na wadau wengine kwa kuwa makini na uhusiano mzuri na wanaotuunga mkono na wahisani.

4. Kutumia utaalamu wetu maalum katika maendeleo endelevu na hatua dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi katika tafiti zetu, programu, na shughuli mbambali ili kusaidia kupambana na janga la tabianchi.

5. Kufuata mbinu ya kimkakati ili kuboresha sifa yetu nzuri sana katika sanaa na utamaduni kimataifa.

# 3: Ushirikiano wa kimataifa

UCC itakuwa mshirika wa kimkakati na wa kimaadili, tukitumia mitandao na washirika wetu kunufaisha dunia.

---

## Hatua za Kipaumbele

## Tumedhamiria

1. Kuunda mfumo wa ushirikiano Katika haki za binadamu, kutangaza mtazamo wetu wa maadili mema na kuwajibika katika ushirikiano wa kimataifa unaoendana na tunu zetu.

2. Kushirikiana na wadau wetu wa kimataifa wa aina mbalimbali ili kuendeleza mkakati wa Chuo na malengo ya Raia wa Dunia 2030, mkakati wa vipaji na ubunifu wa kimataifa wa Ireland.

3. Kutumia mbinu ya kimkakati ya ushirikiano, kushirikiana na vyuo vikuu vinavyoongoza na mitandao maarufu duniani, ili kuendeleza malengo yetu kidunia.

4. Kutumia kikamilifu katika ushirika wetu wa Muungano wa Vyuo Vikuu vya Ulaya, UNIC, kuendeleza ushirikiano wa kina na washirika wetu wa Ulaya na kukiweka Chuo chetu katikati ya Ulaya.

5. Kuipa kipaumbele mikoa na kanda muhimu katika kukuza ushirikiano wa kimkakati katika shughuli zetu zote za ushirikiano wa kimataifa.

# 4: Uraia Mwema Duniani

UCC itaendeleza Uraia mwema wa dunia katika elimu, utafiti na ushirikiano, ili kukuza maelewano mazuri miongoni mwa binadamu

## Hatua za kipaumbele

## Tumedhamiria

1. Kuendeleza zaidi dhamira yetu ya Uraia mwema wa Dunia kwa kuingiza elimu ya maendeleo, ikiwemo Malengo ya Dunia ya Maendeleo Endelevu, katika mtaala wetu na utafiti wetu kwa mujibu wa mtaala wetu unganishi.

2. Kuiinua UCC kama mahali ambapo utambulisho na tamaduni zote zinasherekewa na uelewa wa kiutamaduni unakuzwa, kwa mujibu wa tunu zetu.

3. Kuandaa na kukuza sera ya Lugha kwa Wote ili kuwezesha mafanikio ya wanafunzi, ujumuishi, uwezo wa kwenda sehemu mbalimbali na uelewa wa tamaduni.

4. Kukuza fursa zaidi za ndani na nje za wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa chuo, ikiwa pamoja na kubadilishana kwa watu kwenda au kuja kwetu na pia kwa njia za mtandao wa elektroniki kufanikisha azma ya yetu kujenga uraia mwema na maelewano duniani.

5. Kuimarisha nafasi ya UCC kama Chuo Kikuu cha Ukimbilio (University of Sanctuary), kwa kutimiza wajibu wetu kama raia mwema wa dunia hapa nyumbani na nchi za nje..